



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI

Simu No: +255 (26) 2966008
Fax No:
Email: ded@uyuidc.go.tz

S.L.P. 610,
TABORA.

19 /5 /2021

WANANCHI WOTE

TANGAZO LA KAZI YA KAKUCHANJA MIFUGO

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, leo tarehe 1 9/05/2021 Inawatangazia kazi kwa wazabuni wenye uwezo wa kufanya kazi ,ya Kuchanja mifugo katika Halmashauri ya wilaya Uyui.

WAOMBAJI WOTE WAZINGATIE VIGEZO VIFUATAVYO

1 VIGEZO VITAKAVYOTUMIKA KATIKA KUENDESHA CHANJO YA MAPELE YA NGOZI

- Mzabuni lazima awe na kampuni iliyosajiliwa na Baraza la Veterinari Tanzania kwa ajili ya kutoa huduma za tiba na Kinga ya mifugo
- Awe na mtaji wa kuweza kuendesha kazi ya chanjo mpaka ikamilike
- Mzabuni awe na uzoefu wa kufanya kazi ya chanjo ya mifugo
- Awe na Magari angalau 3 kwa ajili ya kubeba wachanjaji na vifaa
- Awe na Vifaa vya kutosha ikiwa ni pamoja na Sindano, Bomba za sindano, vifaa vya kutunza ubaridi na dawa za kutibu maudhi ya chanjo
- Awe tayari kufanya kazi kwa ubia na Halmashauri
- Atatumia dawa za chanjo zinazokubalika na Mamlaka ya dawa na Vifaa tiba (TMDA) na Kurugenzi ya huduma za Mifugo.

2 WAJIBU WA HALMASHAURI

- a. Halmashauri itawajibika kutoa wataalam **10** kutoka makao makuu ya wilaya na vijijini kwa ajili ya kuendesha na kusimamia zoezi la chanjo.

3

WAJIBU WA KAMPUNI

- a. Kampuni kwa gharama zake itashirikiana na wataalam wa idara ya mifugo, na viongozi wa vyama vya wafugaji kuhamasisha zoezi la chanjo katika kata zote katika hatua za awali na kumwezesha mkuu wa wilaya kwenda kuzindua kampeni ya chanjo.
- b. Kuweka au kujaza aina ya chajo, tarehe na jina la mchanjaji katika daftari la kumbukumbu ya chanjo la mfugaji.
- c. Kampuni itagharamikia ununuzi na utunzaji wa dawa za chanjo ambazo zimethibitishwa na baraza la veterinari Tanzania pamoja na vifaa vingine mfano, sindano, bomba za sindano, majokofu kwa ajili ya kuhifadhia dawa na vifaa vingine ambavyo vitahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi la chanjo.
- d. Kampuni itawajibika kutoa magari matatu (3) na mafuta kwa ajili ya zoezi la chanjo.
- e. Kampuni itawajibika kutumia mashine ya kielektroniki ya kukusanyia fedha pamoja na kutoa risiti za aina mbili yaani ya kielekitroniki na ya mkono kwa kila ng'ombe anayechanjwa.
- f. Kampuni itatakiwa kuwasilisha halmashauri asilimia 10 ya mapato yote kila siku kama mapato ya serikali (majadiliano yanaweza kufanyika pia)
- g. Kampuni itawajibika kuwalipa wataalam 10 (wachanjaji) kutoka Halmashauri posho ya kujikimu kwa kiwango cha nusu ya kulala nje ya kituo cha kazi katika ngazi ya kijiji (half per diem) ambayo ni Tshs 30,000.00 kwa siku kwa kila mchanjaji.
- h. Kampuni itawajibika kuwalipa viongozi wa ngazi ya vijiji pamoja na viongozi wa wafugaji asilimia 5 ya mapato yote kama posho zao na asilimia hiyo itakabidhiwa hapohapo kijijini mara baada ya zoezi la kuchanja.

4

KIWANGO CHA KUCHANJA

- a. Gharama za kuchanja kwa kila ng'ombe mmoja itakuwa ni shilingi mia sita tu (Tshs 600/=)
- b. Muda wa kuchanja Mifugo: Ng'ombe watachanjwa kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni kila siku mpaka siku ya kumaliza zoezi la chanjo. Ikitokea mifugo bado ipo kwenye kibanio zoezi litaendelea hadi saa 12.00

5

UTUNZAJI WA VITENDEA KAZI

5.1 Kampuni itawajibika katika utunzaji wa vifaa vyote vitakavyotumika katika zoezi la chanjo

5.2 Endapo mifugo itapata madhara yoyote yatokanayo na chanjo au uchanjaji, kampuni itawajibika kutoa huduma za matibabu na hasara itakayotokana na chanjo iliotolewa. Isipokuwa kama mfugaji atasingizia bila kuhakikisha kitaalam kuwa mifugo yake imedhurika kwa chanjo na ikabainika kuwa sio kweli, basi mfugaji atawajibishwa kulingana na mkataba huu.

Mwisho wa kupokea maombi ya mafundi ni **tarehe 26/05/2021 Saa 4.00 Asubuhi** na maombi yafungwe kwenye bahasha. Na ufunguzi wa maombi utafunguliwa mara tu muda wa kupokea maombi ukiisha.

Waombaji wote wawasilishe maombi yao katika ofisi ya

AFISA UGAVI NA MANUNUZI

Maombi yote yatapokelewa katika ofisi ya Manunuzi na Ugavi juu ya bahasha andika kwa **Mkurugenzi Mtendaji (W) wa Halmashauri ya Uyui, S.L.P 610, Uyui** andika kazi uliyoomba juu ya bahasha.

Imetolewa na



Hemed S. Magaro
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA UYUI

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

UYUI